

Ni nini ambacho Huelekeza Ufikiaji wa Lugha nchini Marekani?

- Kichwa cha VI cha Sheria ya Haki za Raia, 1964;
- Sheria ya Wamerekani wenye Ulemavu (ADA, 1990)
- Sehemu ya 1557 ya Sheria ya Utunzaji wa Bei Nafuu (ACA,2010); 45 CFR 92.101.

Ni nini kinachoendesha Ufikiaji wa Lugha nchini Marekani?

- Lugha zaidi ya **830** zinazungumzwa nchini marekani
- Watu zaidi ya **67M** nchini Marekani hutumia lugha nyingine mbali na Kiingereza nyumbani
- Watu zaidi ya **26M** wana ufahamu mdogo wa Kiingereza
- Zaidi ya Watu **1M** nchini Marekani ni Viziwi, na zaidi ya **9M** Hawawezi Kusikia Vizuri

Ni nani wanaoathiriwa na sheria za ufikiaji wa lugha na mawasiliano mazuri nchini Marekani?

Ikiwa unafadhiliwa na serikali au uko chini ya ADA, ni lazima utoe ufikiaji wa lugha bila malipo na mawasiliano mazuri kwa watu ambao ni Viziwi, Wale Wasioweza Kusikia Vizuri na LEP.

Ni lugha zipi ambazo zinazungumzwa zaidi nchini Marekani?

Kihispania, Kiarabu, Kichina, Kibengali, Kivietnamu, Kikorea, Kihmnog, Kiukrania, Kidari, Kifarsi, Kipashto na Kipolishi.

Haki za Kisheria

Viziwi na Wasioweza Kusikia Vizuri na watu wenye ujuzi mdogo wa lugha ya Kiingereza wana haki ya kuwasiliana nawe katika lugha wanayoelewa. Msingi wa haki hii ni Kichwa cha VI cha Sheria ya Haki za Raia ya 1964, Sehemu ya 1557 ya Sheria ya Ulinzi wa Mgonjwa na Utunzaji wa Bei Nafuu, Sheria ya Waamerka Wenye Ulemavu, na sheria zingine za jimbo na serikali zinazohusika.

Wajibu wa Kisheria

Ni takwa la kisheria kwamba shirika lolote linalopokea ufadhili wa serikali kwa ajili ya programu zao zozote liweze kuandaa ufikiaji wa lugha unaofaa na mawasiliano mazuri kupitia huduma za ukalimani na utafsiri kwa wale wenye Ujuzi Mdogo wa Kiingereza (LEP), Viziwi na wale wasioweza kusikia vizuri, katika lugha wanayoelewa bila wao kulipa chochote. Una wajibu wa kisheria wa kuandaa ufikiaji huu chini ya Kichwa cha VI cha Sheria ya Haki za Raia ya 1964, Sehemu ya 1557 ya Sheria ya Ulinzi wa Mgonjwa na Utunzaji wa Bei Nafuu, Sheria ya Waamerka Wenye Ulemavu, na sheria zingine za jimbo na serikali zinazohusika.

Jinsi ya Kutimiza Wajibu Huu wa Kisheria

Mashirika yanayofadhiliwa na serikali yanawajibu wa kisheria wa kuandaa mkalimani aliyehitimu wakati ambapo huduma zao zinahitajiwa na wenye Ujuzi Mdogo wa Kiingereza (LEP), Viziwi na Wasioweza Kusikia Vizuri, ili waweze kuwasiliana katika lugha wanayoelewa bila kutozwa ada yoyote. Wajibu wako wa Kisheria chini ya sheria zinazohusika na ufikiaji wa lugha unatia ndani kutafsiri mawasiliano yoyote yaliyoandikwa kwa lugha ambayo vikundi hivi vinaelewa, kutia ndani barua kwa wazazi, notisi, na yaliyomo katika tovuti na mengine. Tafsiri hizi ni sharti zifanywe kwa makini.

Huduma ni sharti zipangiwe, ziratibiwe na kuandaliwa kwa msaada wa mkalimani iwe mahali pa kukutania au kupitia vidio, simu au teknolojia nyingine.

Ili kujifunza zaidi kuhusu haki za ufikiaji wa lugha na matakwa ya kisheria, nenda hapa:

